NA NIKITAKA KUMSHTAKI MTU AMA BIASHARA ILIYONIBAGUA?

Ikiwa ungependa kufuatilia shauri lako mahakamani, unaweza kuzungumza na mawakili walio na ujuzi kuhusu madai ya ubaguzi. Unaweza kuomba ilani ya haki ya kushtaki baada ya mamlaka ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa kusikiliza mamlaka yako kwa siku 60. Hata hivyo, baada ya ilani kutolewa, una siku 90 za kuwasilisha shtaka katika mahakama ya wilaya la sivyo utapoteza haki ya kushtaki.

Tunapendekeza utafute na kujadili na wakili kuhusu muda kabla ya kutuma ombi la kupata ilani ya kushtaki ili uepuke matukio ya muda kuisha unapowasilisha kesi yako katika mahakama ya wilaya.

Tafadhali kumbuka kwamba ilani ya haki ya kushtaki haiwezi kutolewa ikiwa (1) tayari kumekuwa na uamuzi kwamba hakuna sababu ya kushtaki, (2) makubaliano yaliyotokana na usuluhishi yanatekelezwa, (3) tume imemkabidhi mshutumiwa ilani ya kujibu, au (4) malalamiko yamefungwa kutokana na maamuzi ya kiutawala NA miaka miwili imepita tangu muda wa kipindi kinachoruhusiwa kuwasilisha malalamiko.

CITY OF IOWA CITY

TUME YA HAKI ZA BINADAMU
JIJI LA IOWA
410 E. Washington St.
Iowa City, IA 52240
www.icgov.org/humanrights
356-5022 au 356-5015
humanrights@iowa-city.org

FAHAMU HAKI ZAKO

Je, Nimebaguliwa?
Nifanye Nini?

TUME YA HAKI ZA BINADAMU
JIJI LA IOWA
410 E. Washington St.
Iowa City, IA 52240
www.icgov.org/humanrights
356-5022 au 356-5015
humanrights@iowa-city.org

KUPATA FURSA SAWA NA KUTOBAGULIWA NI SHERIA NA NI HAKI YAKO
Ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa, au ikiwa ungependa kupata maelezo zaidi kuhusu aina za ubaguzi uliopigwa marufuku, tafadhali wasiliana na Mshirikishi wa Haki za Binadamu kupitia 356-5022 au Mchunguzi wa Haki za Binadamu kupitia 356-5015.

OFISI YA HAKI ZA BINADAMU INA KAZI GANI?

Wafanyakazi wa Tume ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa wana mamlaka kutoka kwenye Sheria ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa, iliyo chini ya Mada ya II ya Kanuni za Jiji. Wafanyakazi huchunguza malalamiko, huongoza usuluhishi, mapatano, hutekeleza Sheria ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa (na vilevile, vipengele vya sheria za jimbo na za taifa zinazopinga ubaguzi). Pia wanatatua mashauri. Ofisi ya Haki za Binadamu huhusika katika shughuli za uelimishaji, mapendekezo ya sera na shughuli nyingine zinazolenga kukuza usawa katika Jamii ya Jiji la Iowa.

UBAGUZI NI NINI?

Ubaguzi kinyume cha sheria unahusu kumtendea mtu kwa namna isiyo bora akilinganishwa na mtu mwingine, kwa sababu ya sifa zake zinazolindwa, katika hali inayolindwa. Ubaguzi unaweza kufanyika wakati mtu binafsi anapotendewa kwa namna isiyo bora akilinganishwa na mtu mwingine kwa sababu ya sifa zinalolindwa au wakati sera au desturi zinawadhulumu watu kwa sababu ya sifa zinazolindwa.

NA JE, NIKIWA MJAMZITO?

Kubaguliwa kwa sababu u mjamzito ni kinyume cha sheria. Sheria Ubaguzi wa Wajawazito ya 1978 inabainisha kwamba ubaguzi wa ujauzito ni sawa na ubaguzi wa jinsia.

JE, HALI IKIWA MBAYA ZAIDI BAADA YA MALALAMIKO YANGU?

Ni kinyume cha sheria kulipiza kisasi baada ya mtu:

- kulalamikia kubaguliwa,
- kupinga kubaguliwa kwa njia halali, au
- kushirikiana au kusaidia katika uchunguzi wa malalamiko ya mtu mwingine kubaguliwa.

Ikiwa unahisi kwamba unalipizwa kisasi kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa misingi hiyo tu. Pia unaweza kuongeza vitendo vya kulipiziwa kisasi kwenye malalamiko ya awali ya kubaguliwa na kuyawasilisha kwa ofisi hii.

NI NANI ANALINDWA?		VIPENGELE VINAVYOLINDWA				
		Ajira	Nyumba za Serikali	Elimu	Mkopo	Nyumba
SIFA ZINAZOLINDWA	Umri	•	•	•	•	•
	Rangi	•	•	•	•	•
	Imani	•	•	•	•	•
	Ulemavu	•	•	•	•	•
	Hali ya Familia					•
	Utambulisho wa Jinsia	•	•	•	•	•
	Hali ya Ndoa	•	•	•	•	•
	Nchi Ulipotoka	•	•	•	•	•
	Kuwa na au Kukosa Wanaokutegemea					•
	Mapato Yanayotokana na Msaada wa Serikali					•
	Usuli	•	•	•	•	•
	Dini	•	•	•	•	•
	Jinsia	•	•	•	•	•
	Mwelekeo wa Kimapenzi	•	•	•	•	•

NITAPATA WAPI FOMU YA KULALAMIKA?

Unaweza kupata fomu ya kulalamika kwa njia kadhaa:

- Njoo katika Ofisi ya Haki za Binadamu,
- Fungua ukurasa wa malalamiko kwenye tovuti yetu http://www.icgov.org/humanrights
- Piga simu 319-356-5022 au 319-356-5015 na uombe kutumiwa fomu ya malalamiko kwa sanduku la barua.

NI VIPI NITAWASILISHA MALALAMIKO?

Unaweza kuwasilisha malalamiko kwa njia kadhaa:

- Leta fomu ya malalamiko katika Ofisi ya Haki za Binadamu iliyo katika ghorofa ya tatu ya City Hall.
- Kutuma kwa njia ya posta kuja katika Ofisi ya Haki za Binadamu, iliyo 410 E. Washington St., Iowa City, IA 52240.
- Kutuma barua pepe yenye fomu uliyojaza kikamilifu, ikiwa na saini na tarehe kwenda humanrights@iowa-city.org

NANI ANAWEZA KUWASILISHA MALALAMIKO?

Kama huna uhakika ikiwa unatimiza vigezo vilivyotajwa hapa chini, tafadhali piga simu 319-356-5022 au 319-356-5015 ili uzungumze na ofisa wa Haki za Binadamu.

Kwa malalamiko yanayohusu ubaguzi wa ajira, unaweza kuyawasilisha kwa mamlaka ya Haki za Binadamu la Jiji la Iowa ikiwa:

- Unafanya kazi ndani ya mipaka ya kijiografia ya jiji la Iowa, au
- Kazi yako haitegemei eneo mahususi (kwa mfano ikiwa wewe ni muuguzi unayeenda nyumbani kwa wateja, au unafanya kazi kwa kampuni ya ajira ya muda mfupi inayoweza kukutuma katika maeneo mbalimbali mradi kuna kazi) NA ikiwa ofisi ya mwajiri wako ipo katika mipaka ya Jiji la Iowa.

Unaweza kuwasilisha malalamiko kuhusu kubaguliwa katika nyumba za serikali, makazi au huduma za mikopo kwa mamlaka ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa ikiwa:

- Biashara, nyumba au mkopeshaji yupo katika mipaka ya Jiji la Iowa.

Unaweza kuwasilisha malalamiko kuhusu kubaguliwa katika elimu kwa mamlaka ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa ikiwa:

- Malalamiko yanahusu shule iliyo ndani ya mipaka ya Wilaya ya Shule za Jiji la Iowa; au
- Shule katika mipaka ya Jiji la Iowa. (Mfano: Ikiwa taasisi ya elimu ina matawi kadhaa, unaweza kuwasilisha malalamiko ikiwa unahudhuria tawi lililo katika Jiji la Iowa, lakini HUWEZO ikiwa unahudhuria tawi kuu lililo katika jiji lingine.)
- Malalamiko si dhidi ya Chuo Kikuu cha Iowa.

JE, NITAPATA USAIDIZI WAPI IKIWA HALI YANGU HAILINGANI NA MASHARTI YALIYO HAPO JUU?

Tume ya Haki za Umma Jijini Iowa (ICRC) hushughulikia malalamiko katika jimbo zima. Ikiwa umebaguliwa katika miji ya Coralville, North Liberty, au mji mwingine usio na Ofisi ya Haki za Binadamu, wasiliana na ICRC kwa simu 1-800-457-4416. Ili kulalamikia ubaguzi unaotokea kwatika Chuo Kikuu cha Iowa, wasiliana na Ofisi ya Utangamano na Fursa Sawa ya UI kwa simu 319-335-0705.

ITANIGHARIMU PESA NGAPI?

Hutatozwa ada yoyote kwa huduma unazopokea kutoka Ofisi ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa.

NI LINI NINAWEZA KUWASILISHA MALALAMIKO?

Ni sharti uwasilishe malalamiko ndani ya siku 300 tangu kutokea kwa tukio la hivi majuzi zaidi la kubaguliwa unalotaka kulalamikia. Hata hivyo, ni bora uwasilishe ripoti haraka uwezavyo. Ukiwasilisha malalamiko punde baada ya kubaguliwa, kuna uwezekano mzuri wa kupata hati na kwa mashahidi kukumbuka kilichotokea.

JE, NINATAKIWA KUWA NA WAKILI?

Si lazima uwe na wakili ili uwasilishe malalamiko. Ofisi ya Haki za Binadamu hutoa maelekezo na usaidizi wakati wa uchunguzi wa malalamiko lakini HAITOI huduma za kisheria na haifanyi jukumu la uwakili. Unaweza kuajiri wakili kama unapenda, lakini utawajibikia ada zote za wakili.

JE, OFISI YA HAKI ZA BINADAMU YA JIJI LA IOWA INA HUDUMA NYINGINE?

Ndiyo. Tunafanya jukumu la usuluhishi katika malalamiko. Huu ni mchakato wa hiari ambao unaofanywa tu endapo pande mbili husika zimekubali usuluhishi kwa nia njema.
Pia tunafanya mipango ya uelimishaji, huwa tunaandaa Mikutano ya Staftahi ya Haki za Binadamu na Tuzo za Haki za Binadamu kwa Vijana. Pia tunahusika katika shughuli nyingine zinazohamasisha kuondoa ubaguzi katika jamii yetu. Ikiwa ungependa mmoja wetu awasilishe katika shirika au biashara yako, tafadhali piga simu 319-356-5022 au 356-5015.

MCHAKATO WA KUWASILISHA MALALAMIKO